


ESTA



ESTA

Na habari nyingine za wanawake wa Biblia

REBEKA

na

RUTHU



Central Tanganyika Press,
P. O. Box 1129, Dodoma

Copyright © Central Tanganyika Press 1969
Kimetolewa tena 1976, 1981, 1987
ISBN 9976 66 052 9

Kitabu hiki kimeandikwa na D.C.T.
Literature and Christian Education Centre

Picha zimechorwa na Patricia McIntosh

Printed in Tanzania by inland press Box 125, Mwanza ip
4M

ESTA

Zamani kulikuwa na msichana wa Kiyahudi. Alikuwa mzuri sana, jina lake Esta. Esta hakuwaona wazazi wake kwa sababu wao walikufa wakati yeye alikuwa angali mdogo. Lakini alikaa na binamu yake aliyeitwa Mordekai, naye alimpenda kama mtoto wake mwenyewe. Wayahudi hawa walimwamini Mungu aliye hai.

Basi huyu msichana alipofikisha umri wa kuolewa, Mordekai alisikia kuwa mfalme anataka wasichana wengi wakae nyumbani mwake ili achague Malkia. Kwa hiyo Mordekai akaenda mbio nyumbani. Alipofika akamwita Esta, akamwambia, "Esta mwanangu njoo hapa!"

Esta alipokwenda akauliza, "Kuna jambo gani huko?"

Mordekai akamwambia, "Funga vitu vyako vyote kwa sababu mimi nimekutia katika kundi la wasichana watakao-kaa katika jumba la mfalme. Labda mfalme atapendezwa nawe na atakuchagua uwe malkia."



Esta alifurahi sana, akafunga vitu vyake, nguo na kila kitu. Akaenda akajiunga pamoja na wale wasichana walio-kuwa wanakaa kwenye nyumba ya mfalme. Basi alikaa kule, akawa msichana mzuri, akawa anatii na kufuata

maagizo yote. Wasichana wote wali-angaliwa sana na kutunzwa vizuri sana mpaka wakati ulipofika mfalme alikuwa tayari kuchagua msichana atakayempenda. Ikawa kwa zamu,



kila msichana kuingia pole pole wanapokwenda kuji-onyesha.

Walikuwa wanaomba kitu cho chote walichotaka, kama nguo nzuri, viatu, vipuli, ushanga mwingi mzuri, sabuni na mafuta, poda na rangi.

Zamu ya Esta ilipofika yule mlinzi akamwuliza, "Uta-hitaji nini utakapoingia mbele ya mfalme?"

Esta akasema, "Mimi sita-hitaji cho chote."

Basi yule mlinzi alimruhusu akaingia. Na wakati Esta alipoingia mfalme alimtaazama

pamoja na wale wengine waliosimama pamoja naye. Alifurahi sana kuona uzuri wa Esta. Pole pole mfalme aka-inua fimbo yake ya dhahabu, akamwita jina lake. Halafu alisogea, naye mfalme akamvika taji, akamfanya kuwa malkia.

Esta alikaa sana katika jumba la mfalme. Kama ilivyo-kuwa kawaida ya malkia, alikaa ndani tu hakutoka nje ovyo. Na Mordekai aliendelea kufanya kazi yake kwenye jumba la mfalme.



Siku moja Mordekai aliposimama malangoni akasikia watu wawili wakizungumza. Watu hao walikuwa wakimchukia mfalme na walikuwa wanataka kumwangamiza. Basi Mordekai aliposikia hivi akakimbia mbio, akampelekea Esta habari juu ya watu hao wawili. Esta akamwambia mfalme kuwa kuna watu wanaotaka kumfanyia hila. Naye alitaja kuwa aliyemwambia ni Mordekai. Mfalme alikasirika na kumuru wale watu wauawe, jina la Mordekai likaandikwa katika kitabu cha taarifa.

Baada ya siku chache mfalme akapendezwa sana akachukua mmoja wa waziri wake akampandisha cheo akamfanya kuwa waziri mkubwa kabisa. Huyu waziri, Hamani, alipata kiburi sana, kila alipokuwa anatembea aliona hakuna mtu mwingine kama yeye. Alipokuwa akipita watu wote waliinama mbele yake na kuabudu na kumsifu sana.

Lakini huyu Mordekai alipinga jambo hili, hata wakati Hamani akipita alikuwa hainami kwa sababu alisema, "Mimi nitamwabudu Mungu wa kweli tu."

Watu waliomwona Mordekai na kusikia maneno yake walikasirika sana. Wakaenda kumchongea kwa Hamani,

waziri mkuu, kuwa yeye hataki kumwinamia wakati anapopita.

Basi yule Hamani akakasirika kweli kweli, hata usiku ule hakulala kwa ajili ya chuki yake kwa Mordekai. Akasema, "Siwezi kuangamiza Mordekai peke yake, lakini nitaangamiza kabila zima la Mordekai."

Kesho yake alikwenda kwa mfalme kuomba rufusa ya kufanya hivi, na mfalme akatoa sahihi kuwa Wayahudi wote waangamizwe. Alimtanganya mfalme kabisa, akamwambia kuwa watu hawa wote ni waasi, naye mfalme akayatia mambo hayo mikononi mwa Hamani.

Basi Hamani akaandika barua na kutia muhuri wa kifalme. Barua ilisema hivi, "Tarehe ya 13 ya mwezi wa Adari, mwezi wa kumi na mbili, Wayahudi wote waangamizwe."

Wapanda farasi waliingia katika sehemu mbalimbali za ufalme ule kupeleka tangazo alilokuwa ametunga Hamani.

Wayahudi walisikitika kweli, kilio kikubwa kilisikiwa katika ufalme. Walimwomba sana Mungu wao. Wakavaa nguo za magunia, hata Mordekai akalala kwenye mavumbi kabisa, akimlilia Mungu na kusikitika sana. Hakuweza kuingia nyumbani kwa mfalme, akivaa nguo za magunia; lakini watumishi wa Esta walimwona, wakamwambia Esta juu ya huzuni ya Mordekai.

Esta, kwa kuwa ni malkia alikuwa hatoki, na amri hii aliyoitoa Hamani, yeye hakuisikia, wala hakuweza kuonana na Mordekai. Kwa hiyo alimtuma mtumishi aende kwa Mordekai, naye alipomwona huyu mtumishi akimwuliza, alimpa ile nakala ya tangazo la Hamani juu ya kuangamizwa kwa Wayahudi, akamwambia, "Kampe hii Malkia Esta, pia kamwambie kuwa atuongee maisha yetu mbele ya mfalme."

Mtumishi yule akaenda kwa Esta na kumwambia yote.

Kwa kweli wakati ule ilikuwa vigumu sana mtu ye yote kusimama mbele ya mfalme kama hakuitwa. Esta alisema hivi, "Mimi kwa muda mrefu sasa mfalme hajaniita, na nikisimama mbele yake nitauawa. Lakini si kitu. Mwambie Mordekai akusanye Wayahudi wote, wakafunge, na baada ya siku tatu nitaingia kwa mfalme. Yawezekana nitauawa au kama mfalme akipendezwa nami ataniinulia fimbo yake ya dhahabu nami nitapona."

Basi Mordekai akaenda na kuwakusanya Wayahudi, wakafunga kwa siku tatu. Naye Esta na watumishi wake wakafunga siku tatu, hawakula wala hawakunywa.

Baada ya siku tatu Esta akavaa vizuri nguo zake za kifalme, akaenda akasimama mlangoni. Mfalme alikuwa amekaa kwenye kiti chake cha enzi akielekea mlangoni. Alipomwona Malkia Esta akainua fimbo yake ya dhahabu akamwambia, "Karibu Malkia Esta, unataka nini? Ombi lako ni nini? Nitakutumizia, hata nusu ya ufalme wangu naweza nikakupa."



Esta akasema hivi, "Kama ikikupendeza Mfalme, naomba wewe na Hamani mje nyumbani kwangu kwa chakula ambacho nitakiandaa."

Mfalme alifurahi sana kuona anakaribishwa kwa malkia kula chakula.

Jioni Mfalme pamoja na Hamani wakafika chakulani kwa malkia Esta. Wakala wakafurahi. Hata mwisho wa chakula mfalme akamwuliza tena, "Malkia Esta shida yako ni nini tuweze kukutumizia?"

Esta hakusema shida bali alisema, "Shida yangu nitasema kesho, kama Mfalme akipendezwa tena kurudi, yeye na Hamani kwa chakula nitakachokiandaa."

Basi mfalme alifurahi kusikia kuwa anaalikwa tena kwenye maandalio haya kwa malkia. Walikubali na waka-toka mezani.

Usiku ule mfalme hakulala. Alipoingia kitandani mwake hakupata usingizi. Aliagiza mtumishi wake alete kitabu



cha taarifa, amsomee. Yule mtu akaja akaanza kusoma mambo yaliyopita. Alisikia kuwa Mordekai ndiye aliye-wasikia wale watumishi wawili wakizungumza kwa siri wakikusudia kumwua mfalme, na waliuawa. Na saa hiyo mfalme alikumbuka kuwa mtu aliyemfanyia hivyo bila shaka alimpenda.

Alimwuliza yule aliyekuwa akimsomea, "Je, mtu huyu Mordekai tulimpa nini? Tulimtolea asante yo yote?"

Yule mtu akasema, "Hata hatukutoa cho chote."

Basi mfalme akafikiria juu ya habari hii, akataka kumwuliza Hamani, makamu wake. Kesho asubuhi Hamani alifika. Watumishi wakaleta habari kuwa Hamani amekuja, mfalme akamwagiza aingie. Hamani alipoingia ndani mfalme akamwuliza, akasema, "Unafikiri ni jambo gani litafaa kumfanyia mtu ambaye mfalme ataka kumheshimu?"

Hamani alifurahi sana kusikia hivi, akafikiri, "Nani ambaye mfalme atapenda kumpa heshima isipokuwa mimi?" Basi alianza kutaja mambo ya sifa tupu, akasema hivi, "Kwanza mtu huyo avikwe kofia ile ya kifalme ndipo yachukuliwe mavazi mazuri ya kifalme ayavae. Halafu wachukue farasi wa mfalme wamtandike na matandiko ya kifalme na mtu huyo aliye juu ya farasi apitishwe kwenye mabarabara makuu na mmoja wa mawaziri apige mbiu akisema, 'Hivyo ndivyo atakavyofanywa mtu ambaye mfalme ataka kumheshimu!'"


Mfalme kusikia hivi alifurahi sana. Akamwambia, "Nenda, kamfanyie hivi Mordekai."

Hamani aliposikia hivi alikasirika sana, maana Mordekai alikuwa ni adui yake na alimdharau sana. Sasa kumwambia akamtembeze mabarabarani, huku amevaa mavazi ya heshima, yeye hakupendezwa. Lakini afanye nini! Ilikuwa amri ya mfalme! Hamani aliondoka, shingo upande, akafanya vile kama mfalme alivyosema.

Hata aliporudi jioni nyumbani kwake, yule Hamani akawa akimweleza mkewe habari zilizotendeka mchana huo, jinsi mfalme alivyomwudhi.

Hata alipokuwa katika kueleza mtumishi akafika kutoka kwa mfalme kumwita kwa ajili ya chakula kwa Esta. Ingawa alikuwa hana furaha ya kutosha kwa kukaa katika nyumba ya mfalme lakini ilimbidi aende tena.

Ikawa tena wameandaliwa chakula kizuri zaidi kilichopangwa katika meza nzuri, na divai safi ya kifalme. Walipokuwa wakila chakula mfalme akamwuliza tena Esta, "Malkia Esta, hasa ombi lako ni nini?"



Esta alipoona kwamba ni siku ya pili na mfalme yuko katika hali ya kufikiria alisema kwamba, "Ombi langu Mfalme, kama itakupendeza uniokoe maisha yangu na hata ya watu wangu. Kwa sababu tumeuzwa, ili tuangamizwe."

Ndipo mfalme alishtuka na kukasirika sana, akauliza, "Ni nani mtu mwenye mawazo mabaya hivi moyoni mwake?"

Esta hakuogopa kumtaja, akajibu, "Ni huyu Hamani!"

Mfalme akazidi kupata hasira kweli, akatoka nje kwenye bustani yake kwenda kutulia kidogo. Hamani kuona mfalme ametoka, alijua kuwa mfalme amekasirika. Na yeye akajitupa miguuni kwa malkia ili kumwomba msamaha lakini hata hivyo haikuwezekana. Mfalme akarudi tena. Alipomwona miguuni pa Esta alidhani Hamani atamfanyia fujo malkia wake, basi akakasirika zaidi. Akaamuru kuwa Hamani atolewe nje wakamwue.

Naye alimweka Mordekai mahali pa Hamani. Barua ya pili iliandikwa, na Wayahudi waliruhusiwa kupigania maisha yao siku ile ya tarehe ya 13 ya mwezi wa Adari. Nao wapanda farasi waliotumwa na mfalme walienda mbio zaidi siku ile kuzunguka ufalme wake wote na kupeleka tangazo ya kuwa Wayahudi waruhusiwe kuwa huru siku ile.

Hofu iliwaingia maadui wote wa Wayahudi, tena Wayahudi walifurahi kujua kwamba waliokolewa katika hatari yao. Mungu aliwalinda.

Mordekai alifanya kazi ya makamu wa mfalme vizuri sana naye mfalme alizidi kumpenda Esta malkia wake. Kweli Mungu yu tayari kuwaongoza watu wote wenye moyo wa kufuata mapenzi yake.

REBEKA

Hapo zamani za kale, walipokuwa wakiishi babu zetu Ibrahimu na Isaka, kulikuwa na msichana aliyekuwa na sura nzuri sana ya kupendeza, jina lake Rebeka. Aliishi Mesopotamia, mji wa Harani.

Siku moja Rebeka alipotumwa kwenda kuteka maji, alimkuta msafiri mmoja aliyewapigisha magoti ngamia zake karibu na kisima cha maji, jina lake Eliezeri.

Rebeka alikuwa na mtungi begani mwake. Eliezeri akamwambia, "Tafadhali unipe maji kidogo katika mtungi wako ninywe." Rebeka hakukawia, aliteka maji upesi akampa, na akamwambia, "Nitawanyweshwa na ngamia pia." Pale pale aliteka maji mengi na kuyamwaga katika birika, mpaka alipowanyweshwa ngamia wote.



Eliezeri alimkazia sana macho, huku akijiuliza mwenyewe kama Bwana amemfanikisha katika safari yake au sivyo. Alipoona kuwa ngamia wote wamekwisha kunywa, alitwaa pete ya dhahabu, na bangili za mkononi akamvika mara. Akamwuliza, "Wewe ni binti wa nani? Je, kuna nafasi katika nyumba ya baba yako, ili mimi na ngamia zangu tupate mahali pa kukaa kwa muda?"

Rebeka akashangaa lakini akajibu, "Mimi ni binti wa Bethueli, mwana wa Milka. Tena kuna majani ya kutosha na mahali pa kukaa wageni." Mara akapiga mbio mpaka nyumbani kwa mama na baba, akawaambia mambo yote yaliyotokea alipokwenda kuteka maji.

Rebeka alikuwa na kaka yake jina lake Labani. Naye aliposikia maneno haya na alipoiona ile pete na bangili ziking'aa mkononi mwa dadake, alijua kuwa anapata shemeji. Kwa hiyo alitoka haraka kwenda kumpokea



Eliezeri kisimani. Alipofika alimkaribisha akimwambia, "Karibu wewe uliyebarikiwa, nimekwisha iweka nyumba tayari na nafasi ya ngamia zako pia". Wakaondoka wote mpaka nyumbani, na pale walikaribishwa vizuri sana.

Chakula kilipoandaliwa na kuwekwa mezani, Eliezeri aliomba rufusa ya kusema maneno yake kabla ya kula kile chakula. Wale wazee walimrufusu.

Naye akasema, "Mimi ni mtumishi wa Ibrahimu, na bwana wangu amejaliwa kupata mali nyingi, mifugo na vijakazi wengi sana. Yeye na mkewe Sara walipata bahati ya kuzaa mtoto mmoja tu katika uzee wao, jina lake Isaka.



"Ibrahimu alipoona kuwa siku za kufa kwake zina-
karibia aliniapisha akiniambia, 'Usimtafutie mwanangu mke
wa binti za Wakanaani ila uende mpaka nyumbani kwa
babangu na kwa jamaa zangu ukanitafutie mwanangu mke.'

'Nami nikamwambia, 'Pengine huyo mwanamke hata-
kubali kufuatana nami.' Lakini yeye alisema kuwa Bwana
aliyemtoa katika nyumba ya baba yake, atanifanikisha
katika njia yangu.

'Leo nikaja kisimani nikamwomba, 'Ee Mungu wa
Bwana wangu Ibrahimu tazama nimesimama karibu na
kisima cha maji, basi na iwe hivi; msichana nitakaye-
mwomba maji, naye akanipa na kuwanyweshwa ngamia zangu
awe ndiye uliyemchagulia.' Muda si mrefu akatokea Rebeka
na mtungi begani mwake, nikamwomba maji naye aka-
nitekea mimi na kuwanyweshwa ngamia zangu pia.

"Sasa niambieni mawazo yenu, ili nijue la kufanya,
kama itanibidi kugeukia
upande wa kuume au wa
kushoto."

Labani na Bethueli wa-
kajibu wakisema, "Neno
hili limetoka kwa Mungu,
kwa hiyo sisi hatuwezi
kukuambia neno zuri au
baya. Rebeka huyo hapo
mbele yako, mchukue tu
awe mke wa mwana wa
Bwana wako kama Mungu
alivyosema."

Eliezeri akainama na
kumshukuru Mungu kwa
jinsi alivyomfanikisha
katika safari yake.



Eliezeri alimpa Rebeka vyombo vya
dhahabu na mavazi mazuri yanayong'aa.
Alitoa vitu vingine vya thamani kubwa
kwa jamaa nzima pia. Siku hiyo wali-
sherehekea vizuri sana, vyakula vili-
pikwa na vinywaji viliandaliwa kwa
wingi sana. Walishangilia na kufurahi
pamoja, wakiimba na kucheza.

Asubuhi, siku ya pili yake Eliezeri
aliomba ruhusa ya kuondoka kurudi kwa
bwana wake. Rebeka aliitwa na
kuulizwa kama atakwenda naye siku
ile ile, naye alijibu, "Nitakwenda."



Wazazi wake walipoona kuwa amekubali, walimwita ili wambariki. Wakamwambia, "Ndugu yetu, uwe mama wa kumi elfu mara elfu nyingi, na wazao wako waurithi mlango wa hao wawachukiao."

Ijapokuwa Rebeka hakupenda kuwaacha jamaa zake, alikubali kusafiri nchi za mbali kwenda kuolewa na mtu asiyemfahamu. Alipewa vijakazi na yaya mmoja jina lake Debora.

Isaka alikuwa amefiwa na mama yake, kwa hiyo alisikia upweke sana. Aliona kama siku zinachelewa, kwa sababu alikuwa akingoja kwa hamu bibi-arusi wake afike wapate kukaa pamoja na kufurahi.

Siku moja aliona vumbi kubwa sana, akajua kuwa bibiye anafika, kwa hiyo alifanya haraka kwenda kuwapokea.

Rebeka alipoinua kichwa, alimwona mtu anayewa-kimbilia akauliza, "Ni nani huyu anayekuja kutupokea?"

Eliezeri akamwambia, "Huyu ndiye atakayekuwa mume wako."

Rebeka alitwaa shela yake akajifunika uso wake, ili asionekane, kwa sababu ilikuwa desturi yao, bibi-arusi kujifunika uso wote mpaka baada ya sherehe za arusi.

Walipofika, Isaka alimchukua Rebeka na kumwingiza katika hema ya mama yake Sara, akawa mkewe akampenda sana.

Kulikuwa na karamu kubwa sana na vipochopocho vingi vilitayarishwa kwa wingi mno. Sherehe nyingi zilifanyika kwa siku chache.

Rebeka aliishi katika hema ya Sara, akafanya kazi zote kama ilivyokuwa kawaida ya wanawake wengine wote wa wakati ule. Mungu alimbariki, akazaa mapacha, nao Rebeka na Isaka walifurahi na kumshukuru Mungu aliyewapenda na kuwaongoza.

RUTHU

Hapo zamani za kale katika Bethlehemu kulikuwa na mtu mmoja Elimeleki, na mke wake Naomi. Walikaa, wakazaa watoto wao wawili, Maloni na Kilioni. Hawa jamaa walimpenda Mungu sana.

Basi ikatokea njaa kubwa katika nchi yao, nao wakakosa chakula kabisa. Hata waliposikia habari nzuri kwamba katika nchi ya Moabu kuna chakula Elimeleki akasema na mkewe na wanawe, "Na tuondoke basi, tuvuke ng'ambo hata huko Moabu, ili tujipatie chakula." Hao, wakafunga vitu vyao, wakaondoka, wakaenda mpaka nchi ya Moabu, wakakaa huko.

Na baada ya muda Elimeleki baba yao akafa. Akamwacha Naomi na watoto wake. Wakajisikia ukiwa sana kufiwa na baba yao.



Maloni na Kilioni wakakua, hata walipokuwa watu wazima walianza kutafuta wanawake wa kuoa. Maloni alimwoa Ruthu na Kilioni akamwoa Orpa, hawa wasichana walikuwa wenyeji wa Moabu. Wakakaa kwa furaha pamoja na mama yao Naomi. Baada ya muda wa miaka kama kumi hivi Maloni na Kilioni wakafa. Ikawa huzuni kubwa sana kwa Naomi na wakwe zake, Ruthu na Orpa. Wameachwa ukiwa tena, zaidi ya hayo, walikuwa wamebaki wanawake watupu. Hakuna mwanamume wa kuwasaidia.

Ndipo baada ya muda Naomi akawa



na mawazo ya kurudi kwao. Alitaka kujua habari za kwao Akapeleleza na kuwauliza wafanya biashara apate habari. Akasikia kwamba nchi yake ilikuwa na vyakula vingi. Basi akakata shauri kurudi Bethlehemu. Kisha Naomi akawaeleza Ruthu na Orpa juu ya shauri hili, na akawaambia, "Nendeni sasa kila mmoja nyumbani kwa mama yake; mkakae kwa raha." Lakini wao wakang'ang'ania kwenda naye. Aliwashawishi sana akisema, "Mimi naenda nyumbani kwetu nilikotoka. Kwa hiyo na ninyi inawapasa kurudi kwenu, kwa sababu kule kwetu hawatawafahamu." Hata hivyo hawakukubali, walikataa wakisema, "Sisi tutakwenda pamoja nawe, hatuwezi kukuacha."

Ndipo wakaondoka wote kuelekea Bethlehemu. Njiani Naomi alizidi kuwasihia sana warudi. Baadaye Orpa alikata shauri kurudi, lakini Ruthu alikataa akasema, "Mimi sitakuacha, uendapo na mimi nitakwenda, utakapokaa nami nitakaa hapo, wala sitakuacha. Na Mungu wako atakuwa Mungu wangu." Basi Naomi alipoona kuwa Ruthu amekaza nia yake ya kufuatana naye, aliacha kumsihia zaidi. Orpa alirudi kwao, bali Ruthu alikwenda Bethlehemu na Naomi.



Wakasafiri, wakafika Bethlehemu. Walipofika walikuwa kama wageni maana Naomi alikuwa ameondoka kwa miaka mingi. Walikaribishwa vizuri, nao walifurahi. Naomi hakukawia kuwaeleza yote



yaliyompata na huzuni zote; hata akawaambia, "Sasa msiniite Naomi tena bali niiteni Mara, maana mimi ni mwenye uchungu sana."

Wakapata mahali pa kukaa, lakini walikuwa hawana shamba. Na Ruthu alijitolea kwenda kuokota shayiri inayobakia nyuma kwa wanaovuna mashambani. Basi akatafuta mashamba watu wanakovuna. Akaenda kwenye shamba la tajiri mmoja aliyekuwa na wafanya kazi wengi. Akawaomba, "Je, naweza kuwa naokota huko nyuma?" Wakamkubalia. Naye akawafuata, akaanza kuokota masazo ya shayiri.

Baadaye mwenye shamba jina lake Boazi, alifika, akaangalia kazi, akaona kuna msichana mgeni anayeokota nyuma. Akamwuliza aliyekuwa akisimamia kazi, "Huyu ni nani?" Akasema, "Ni yule msichana aliyekuja na Naomi.



Kwa kuwa wao hawana shamba yeye amekuja kuokota masazo ya nyuma."

Pale pale Boazi alimtambua kuwa wa jamaa yake, kwa kuwa yeye alikuwa ndugu ya Elimeleki, mume wa Naomi. Kwa hiyo alimpenda sana yule msichana. Akamkaribisha kwa moyo wote, akamwambia, "Usiogope, endelea kuokota shambani mwangu. Ukiwa na njaa unaweza kupata chakula hapa, na ukiwa na kiu unaweza kunywa pamoja na wasichana wangu, wala usiende kwenye shamba lingine."

Basi Ruthu aliona furaha moyoni mwake kusikia maneno haya yenye huruma. Akaendelea kuokota, wakati wa chakula wakamkaribisha, wakala naye. Jioni aliporudi nyumbani akamwonyesha Naomi mavuno haya yote aliyo-pata. Naomi alishangaa akamwuliza, "Ulipata wapi

chakula kingi namna hii?" Ndipo Ruthu alieleza yote juu ya huruma za Boazi.

Naomi alisema, "Kweli Mungu amekuongoza. Huyo ni jamaa yetu, usiogope. Bila shaka Mungu atakufanikisha mapenzi yake."

Kwa hiyo Ruthu aliendelea kuokota masazo ya shayiri shambani mwa Boazi mpaka mwisho wa mavuno. Naye Boazi aliendelea kumwonyesha upendeleo.

Baadaye Naomi akamtuma Ruthu aende kwa Boazi akamwombe awafanyie kama impasavyo jamaa, yaani awatunze. Basi Ruthu alivaa nguo nzuri za kupendeza, akaondoka akaenda kwa Boazi. Boazi akasikiliza kwa makini shida yake. Naye alipofikiria juu ya uaminifu wa Ruthu katika kazi yake, akampenda, akakata shauri kumwoa Ruthu. Ndipo aliwaita wazee wa Waebrania kama ilivyokuwa desturi, akafikisha maneno mbele yao, wakawa kama mashahidi. Baada ya mazungumzo, wakakubaliana, kisha Boazi akamwoa Ruthu.

Mungu aliwabariki wote, Ruthu akamzaa mtoto ambaye walimwita Obedi. Obedi alimzaa Yese, baba ya mfalme Daudi. Na katika jamaa yake Daudi Yesu Mwokozi wa ulimwengu wote, alizaliwa. Kweli Mungu aliwabariki wote kwa sababu ya uaminifu wake Ruthu.





ISBN 9976 66 052 9